THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

*MUDA: Saa 2* *Alhamisi, 15 Oktoba 2009 mchana*

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B, C, D** na **E**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Mashine za hesabu za electronic **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.




Karatasi hii ina kurasa 8 zenye maandishi.

Scanned by CamScanner

## SEHEMU A: (Alama 10)
## SUNNAH NA HADITH

1. Chagua jibu sahihi katika maswali (i) – (x) kisha uandike herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Maelezo yanayotoa tofauti kati ya Sunnah na hadithi ni
A Sunnah ni matendo ya Mtume (s.a.w) ambapo hadithi ni maneno yake
B Sunnah ni mwenendo na mafundisho ya utume wake wakati hadithi ni taarifa za maswahaba juu yake
C Sunnah ni mwenendo, mafundisho na maelekezo ya Mtume (s.a.w) wakati hadithi ni taarifa juu ya Sunnah yake
D Sunnah ni matendo ya Mtume (s.a.w) ambapo hadithi ni simulizi juu ya Sunnah ya Mtume (s.a.w)
E Sunnah ni mambo ya hiari kuyatekeleza wakati hadithi ni hekaya za paukwa pakawa.

(ii) *"Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa" (3:132)..... na Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni katika walioamini kweli." (8:1)*
Jambo kubwa linaloainishwa katika aya hizi ni
A kumfanya Mtume (s.a.w) kiigizo cha maisha yetu ya kila siku
B tumpende Allah (s.w), Mtume (s.a.w) na dini yake kuliko nafsi zetu
C kumtii Mtume (s.a.w) ni sehemu ya imani ya Kiislamu
D *"Na anachokupeni Mtume (s.a.w) basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho" (59:7)*
E kumtii Allah (s.w) kumeambatanishwa na utii kwa Mtume (s.a.w).

(iii) Hadithi zilianza kuwekwa katika maandishi wakati wa
A Maswahaba
B Mtume (s.a.w)
C Tabiin
D Tabiin Tabiin
E Umar bin Abdul-Aziz.



late print uk

Scanned by CamScanner

(iv) Vitabu mashuhuri vya hadithi vinavyotegemewa na Waislamu hujulikana kama **sahih sitta** kwa sababu

A waandishi wake walivipa vitabu hivyo jina hilo

B waandishi wa vitabu hivi hawakuandika hadithi ila iliyopokelewa na watu zaidi ya wanne

C waandishi wa vitabu hivi wamekusanya hadithi zenye kukidhi mahitaji yote ya maisha ya Muislamu

D waandishi wa vitabu walihakikisha hadithi inakidhi vigezo vya Isnad na Matin kabla ya kuandika

E waandishi wote walikuwa wachamungu kweli kweli.

(v) Jambo ambalo halimo katika hadithi ya mambo saba yenye kuangamiza ni

A kumshirikisha Mwenyezi Mungu

B kucheza kamari

C kula riba

D kufanya uchawi

E kula mali ya yatima.

(vi) Moja ya matatizo yaliyotatuliwa kwa kutumia hadithi za Mtume (s.a.w) katika kipindi cha maswahaba ni

A uandishi wa Qur'an wakati wa Uthman (r.a)

B tatizo la Ali (r.a) na Myahudi

C zilipojitokeza tofauti za usomaji wa Qur'an

D Bibi Fatuma (r.a) alipodai mirathi ya baba yake

E uchaguzi wa khalifa wa kwanza wa Mtume (s.a.w).

(vii) Vitabu ambavyo hadithi zake zinategemewa na Waislamu wengi sana ni

A Sahihi Al-Bukhar na Sunnan Abud Daudi

B Sahihi Al-Muslim na At-Tirmidh

C Sunnan ya Abu Daud na Ibn Majah

D Jami'u at-Tirmidh na Bukhar

E Sahihi ya Muslim na Bukhar.

(viii) Hadithi iliyo na Matin sahihi lakini wasimuizi wake si wadhibitifu huitwa

A Sahihi

B Hassan

C Dhaifu

D Maudhuu

E Ahad.

(ix) Isnad ni sehemu ya hadithi inayoonesha

A msururu wa hadithi na majina ya wapokezi wake

B wapokezi kuanzia wale walioishi wakati wa Mtume (s.a.w)

C msururu wa wapokezi toka aliyemuona au kumsikia Mtume (s.a.w)

D msururu wa wapokezi tokea kwa maswahaba wa Mtume (s.a.w)

E msururu wa wapokezi wa hadithi na historia ya maisha yao.



Scanned by CamScanner

(x) Ibn Hajar Al-Asqalan ni mmoja wa wanachuoni wa kipindi cha Tabi Tabiin waliozama katika

A elimu ya Hadithi
B ukusanyaji wa hadithi
C kufutu mas-ala ya kifiqh kwa kutumia hadithi
D kukusanya hadithi na kuzitekeleza katika matendo
E kufutu mas-ala ya Kiislamu kwa hoja na Qiya.

## SEHEMU B: (Alama 15)
## QUR'AN

2. Chagua kutoka orodha B kifungu cha maneno kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka orodha A. Vifungu kutoka orodha B vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

**ORODHA A:**

(i) Hatukukuteremshia Qur'an ili upate mashaka. Bali iwe mawaidha kwa wenye kumyenyekea Mungu (20:2-3).
(ii) Kwa yakini shetani ni adui yenu, basi mfanyeni adui kwani analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni (35 :6).
(iii) Na bila shaka una tabia njema kabisa (68 :4).
(iv) Na waliscma waliokufuru: "Msisikilize Qur'an hii (inaposomwa, isije ikakupotezeni) na ipigieni makelele (isomwapo); huenda mkashinda (akawachilia mbali hum uzushi wake)" (41:26).
(v) Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana (33 :21).
(vi) Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu; na waliopewa elimu watapata daraja zaidi. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote (58 :11).
(vii) Amemfundisha mwanadamu mambo aliyokuwa hayajui (96 :5).
(viii) Kuwa hii (Qur'an) ni kauli ipambanuayo haki, wala si mzaha (86 :13-14).
(ix) Aysha (r.a) amesimulia: "Kwa hakika niniemuona Mtume akiteremshiwa Wahyi siku ya baridi kali na baada ya kumaliza kile kipande cha kuteremshiwa Wahyi alimiminikwa na jasho jingi kichwani mwake. **(Malik)**
(x) Na ukitaka kusoma Qur'an piga Audhubillah (kwanza, jikinge) kwa Mwenyezi Mungu (Akulinde) na shetani aliyefukuzwa (16 :98).
(xi) Na ikapigwa juu yao (chapa ya) dhila (unyonge) na umaskini; na wakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu: Na haya ni kwa sababu walikuwa wakiyakataa maneno ya Mwenyezi Mungu, na wakiwaua Manabiii pasipo haki. Basi haya ni kwa sababu ya kuasi kwao na kupindukia mipaka (ya Mwenyezi Mungu) (2 :61).


tata print uk
Scanned by CamScanner

(xii) Bibi Aysha (r.a) alisema : "Kilichoanza katika Wahyi wa Mtume ni ndoto za kweli. Alikuwa Mtume (s.a.w) haoti chochote isipokuwa hutokea kama alivyoota."

(xiii) Wakasema makafiri : "Hayakuwa haya ila ni kiini macho" (10 :2).

(xiv) Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, wale wasioogopa kukutana Nasi husema : "Lete Qur'an isiyokuwa hii" (10 :15).

(xv) Na haiwezekani kuwa hii Qur'an imetungwa, haitokani na Mwenyezi Mungu. Bali inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya Vitabu (vilivyopita). Haina shaka kuwa imetoka kwa Mola wa walimwengu (wote) (10 :37).

**ORODHA B :**

A Elimu ina nafasi ya kwanza katika Uislamu.
B Upinzani dhidi ya Qur'an ni mkongwe.
C Mtume ndio kiigizo cha Muislamu.
D Al-Fatiha (1 :5-7).
E Qur'an ni neno la Mwenyezi Mungu.
F Tahadhari dhidi ya shetani.

MAKTABA YA SKULI YA NYUKI
Tarehe .....
ZANZIBAR

**SEHEMU C; (Alama 15)**
**TAWHIID**

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Uislamu ndiyo Dini iliyo sawa sawa na ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia binadamu kwa mujibu wa Qur'an (30:30)
  (i) Hiyo ndiyo Dini iliyo ya haki,
  (ii) Ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu
  (iii) Basi uelekeza uso wako katika Dini iliyo sawa sawa
  (iv) Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu.
  (v) lakini watu wengi hawajui.

(b) Ujio wa Mitume wa Allah (s.w) baada ya Nabii Adamu (a.s) ni kama ifuatavyo
  (i) Yaakub (a.s) akifuatiwa na Yusuf (a.s) baada yao
  (ii) Hud (a.s) akifuatiwa na Salehe (a.s), baada yao
  (iii) Ismail (a.s) akifuatiwa na Is-haq (a.s), baada yao
  (iv) Ibrahim (a.s) akiambatana na Lut (a.s), baada yao
  (v) Idris (a.s) akifuatiwa na Nuhu (a.s) baada yao



Scanned by CamScanner

(c) (i) Hakika mwanadamu ametunukiwa akili ili aweze kumyakinisha Allah (s.w) na kumtii ipasavyo.

(ii) Katika Uislamu kumuamini Allah (s.w) si suala la kibubusa.

(iii) Hakika vinyama viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni hawa wanaojipa uziwi wa (kutosikia haki), wanaojipa ububu (wasiikiri hiyo haki), ambao hawayatii akilini (wanayoambiwa) bali huyakataa tu bila kuyapima kwanza. (8 :22)

(iv) Kuna alama nyingi tu katika ulimwengu na mafundisho ya Mitume zinazothibitisha kuwepo kwa Allah (s.w).

(v) Kwa hiyo mwanadamu asiyemkiri na kumtii Allah (s.w) hana tofauti na mnyama kwa mujibu wa Qur'an.

## SEHEMU D: (Alama 30)
## FIQH

4. Jibu kwa ufupi kwa kujaza nafasi zilizo wazi katika swali la (i) – (xv). Andika neno au maneno yanayokosekana tu katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Shahada ya kweli ni ile inayotamkwa kutoka _____ na kudhihirishwa katika _____ ya kila siku.

(ii) Nguzo za swala ya maiti ni (a) nia (b) kusimama mpaka iishe swala (c) _____ (d) _____ na (e) kutoa salamu.

(iii) Kibla cha sasa cha ummah huu wa Mtume Muhammad (s.a.w) ni _____ kibla cha mwanzo kilikuwa _____.

(iv) Nguzo za swala zimegawanyika makundi yafuatayo:
(a) Nia (b) _____ (c) _____ (d) kufuata utaratibu.

(v) Benki za kitwaghuuti huendeshwa katika mfumo wa malimbikizo ya (a) _____ wakati Benki za Kiislamu huendeshwa kwa misingi ya (b) _____.

(vi) Kwa mujibu wa Qur'an, masharti mawili ya Hija ni (a) _____ na (b) _____.

(vii) Matendo ya ibada ya Hija yanayopandikiza hisia za umoja, upendo, undugu na usawa ni:
(a) _____ (b) Ihram (Nia) (c) Tawaf (d) Sai na (e) _____.

(viii) Kwa mujibu wa Qur'an, mahari yametajwa kama (a) _____ anayotoa mume muoaji kumpa (b) _____.

(ix) Kwa mtazamo wa Kiislamu talaka ni (a) _____ inayochukiza mbele ya (b) _____.

(x) Miongoni mwa haki zinazofungamana na mali ya urithi ni (a) zakat (b) _____ na (c) _____.

(xi) Kwa mujibu wa Qur'an, fungu la urithi la mama mzazi wa marehemu ambaye ameacha watoto wa kike na mtoto wa kiume kama warithi pekee ni (a) _____ ya mali ya urithi baada ya kutoa Usia na (b) _____.



tafa print u

Scanned by CamScanner

(xii) Misingi ya sheria ya Kiislamu ni (a) Qur'an (b) Sunnah (c) _____ (d) _____.

(xiii) Kwa mtazamo wa Uislamu, maadili mema hupatikana kwa kufuata barabara mwongozo wa (a) _____ na (b) _____.

(xiv) Na nani atajitenga na mila ya Ibrahim isipokuwa ameitia nafsi yake katika upumbavu? (2:130) Mila ya Ibrahim ni (a) _____ ambayo ndiyo mila ya (b) _____.

(xv) Msonge wa uongozi katika jamii yoyote ya Kiislamu ni huu ufuatao (a) _____ (b) Mtume (s.a.w) (Sunnah) (c) _____ (d) Ulul-Amir (e) Raia.

## SEHEMU E: (Alama 30)
## TAREKH

Chagua neno au **kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili kukamilisha kauli (a) – (o) kwa usahihi.

**Tanbihi:** Neno linaweza kutumika zaidi ya mara moja.

**Maneno au vifungu vya maneno**

(i) Surat Bani Israil
(ii) Katiba ya Madinah
(iii) Hudaibiya
(iv) Qadhi
(v) Umoja
(vi) Kuunda Ummah
(vii) Utume
(viii) Kuwabashiria watu pepo
(ix) Kusimama usiku kuswali
(x) Kuwahofisha watu na moto
(xi) Tanganyika
(xii) Faradhi
(xiii) Aqaba
(xiv) Uhud
(xv) Utii kwa Allah na Mtume wake
xvi) Mtume
(xvii) Swala
(xviii) Udhaifu wa imani
(xix) Ikhlas
(xx) Tamaa ya kipato cha dunia
(xxi) Kumuonesha Mtume baadhi ya alama za Mwenyezi Mungu
(xxii) Kumuwezesha kukubalika
(xxiii) Magumu
(xxiv) Makafiri
(xxv) Kumtukuza Mwenyezi Mungu
(xxvi) Mkataba
(xxvii) Amil

**Maswali**

(a) Sababu za kuletwa Mitume ni _____ na _____.

(b) Misingi ya awali ya kulingania Uislamu aliyopewa Mtume (s.a.w) ni pamoja na _____ na _____.

(c) Kazi ya msingi iliyofanywa na mafunzo ya Ilhamu kwa Mtume kabla ya kupewa _____ ni _____.

(d) _____ waliyoyakabili Waislamu wa Makka wakati wa Mtume (s.a.w) yanatoa fundisho la _____ kwa Waislamu wa leo.



Scanned by CamScanner

(e) Sababu ya safari ya Mtume ya Isra kama inavyobainishwa katika _____ ni _____.

(f) _____ na _____ ni miongoni mwa Taasisi za kisiasa alizozitumia Mtume (s.a.w) kuanzisha serikali ya Kiislamu.

(g) _____, _____ na walii vilikuwa vyeo vya viongozi wa mikoa wa Serikali ya Kiislamu wakati wa Mtume (s.a.w) na wakati wa Makhalifa.

(h) _____, _____ ndiyo mambo muhimu ya msingi yaliyopelekea Waislamu kushinda.

(i) _____ ni mchango mkubwa wa Uislamu katika kuitengeneza _____.

(j) Miongoni mwa sababu zilizopelekea Waislamu wengi kuuhama Uislamu mara tu baada ya kutawafu Mtume ni _____ na _____.

(k) _____ ni moja ya nguzo za Uislamu isiyoamrishwa aridhini na huchukuliwa kama ni _____ ili kumtofautisha Muislamu na Kafiri.

(l) Mikataba miwili ya kisiasa iliyofanywa kati ya _____ na watu wa Yathrib kabla ya Hijra ni _____.

(m) Funzo kubwa kutoka katika vita vya _____ ni kuwa hapana mafanikio pasipo _____.

(n) Fundisho wanalolipata wanaharakati wa Kiislamu kutokana na vita vya _____ ni kuwa _____ wataendelea kuukandamiza Uislamu.

(o) _____ ndiyo katiba ya kwanza kuandikwa duniani ambayo imeandikwa na _____.



lata print u

Scanned by CamScanner